



**TAARIFA KWA UMMA**  
**MKUTANO WA TAFTISHI YA UDHIBITI WA BEI YA MAFUTA**  
**YA PETROLI**

**TAARIFA INATOLEWA KWA** umma na wadau wote wa sekta ya Mafuta ya Petroli (wafanyabiashara, wamiliki wa miundo mbinu, watoa huduma, walaji na taasisi za Serikali) kuwa EWURA inafanya taftishi kuhusu jinsi ya kudhibiti bei ya Mafuta ya Petroli. Taftishi hii inafanyika kwa mujibu wa vifungu Namba 3 na 4A vya Sheria ya Mafuta ya Petroli Sura Namba 392 ya Sheria za Tanzania na kifungu Namba 19 cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Kutokana na utangulizi tajwa hapo juu, wadau wa sekta ya Mafuta ya Petroli na umma wote wanakaribishwa kwenye mkutano wa taftishi utakaofanyika siku ya tarehe 10 mwezi Desemba 2008 katika chumba Namba Mbili (2) Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam. Ajenda ya taftishi ni:

**“UDHIBITI WA BEI YA MAFUTA YA PETROLI TANZANIA”**

Mtu yeyote mwenye nia ya kushiriki (kwa kuunga mkono au kupinga) hatua ya EWURA ya kudhibiti bei ya Mafuta ya Petroli kwa kutoa hoja anapaswa kujiandikisha na kuwasilisha hoja hizo EWURA kabla ya tarehe 5 mwezi Desemba 2008 saa kumi na moja jioni. Ni wale tu watakaokuwa wamejiandikisha ndio watakaoruhusiwa kutoa hoja zao kwa maandishi kwenye taftishi hiyo. Wale watakaoshindwa kujiandikisha watapewa muda wa kutoa maoni yao kwa mdomo au maandishi siku ya taftishi. Wakati wa taftishi hiyo EWURA itakusanya maoni ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri wa Watumia Huduma za EWURA (EWURA CCC) na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC).

Rasimu ya Kanuni za Udhubiti wa Bei ya Mafuta ya Petroli yaani EWURA (Petroleum Products Price Setting) Rules, 2008 na Kanuni ya Upangaji wa Bei ya Mafuta ya Petroli (Petroleum Products Pricing Formula), zinapatikana ofisi za EWURA kwenye anuani tajwa hapa chini au kwenye mtandao wa EWURA yaani [www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)

**KWA MAELEKEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**  
**Mtaa wa Samora, Ghorofa ya Sita, Harbour View Towers**  
**(Zamani JM Mall Building)**  
**S.L.P 72175, DAR ES SALAAM**  
**Simu Na: +255-22-2123850; 2123853; 2123854; 2123856**  
**Nukushi Na: +255-22-2123180**  
**Barua Pepe; [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)**